# <u>SOMO LA KWANZA:BIBLIA-NI NINI.</u>

Je, ni kusudi lake Mungu kutupendeza au ni kusudi letu kumpendeza Mungu? Hili ni mojawapo ya maswali muhimu ya kuzingatia unapojifunza Biblia.

***"Utakuja wakati ambapo watu hawatasikiliza mafundisho ya kweli, ila watafuata tamaa zao wenyewe na kujikusanyia walimu tele watakaowaambia mambo yale tu ambayo masikio yao yako tayari kusikia." ( 2 Timotheo 4:3-4)***

***"Hata kutoka miongoni mwenu watatokea watu ambao watasema mambo ya uongo ili kuwapotosha watu na kuwafanya wawafuate wao tu."( Matendo ya Mitume 20:30)***

***"Bali chunguzeni kwa makini kama huyo mtu anaongozwa na Roho wa Mungu au la, maana manabii wengi wa uongo wamezuka ulimwenguni."(1 Yohana 4:1)***

***"Mafundisho ya aina hiyo ni kama donda linalokula mwili." (2 Timotheo 2:17)***

***"Mataifa yote yalipotoshwa" (Ufunuo wa Yohana 18:23)***

Vifungu hivi, vilivyonukuliwa kutoka kwa Neno la Mungu, vipo kama onyo kwa watu wote kuwa wengi wa wanaojiita "Wakristo" watauwacha Ukweli wa Mungu. Tunatahadharishwa pia kuwa hatupaswi kuwacha maagizo kuhusu mapenzi ya Mungu kwa kikundi kidogo kiitwacho "Wachungaji": mapadri na makuhani. Njia ya pekee kwetu iliyo salama na ya kimaandiko ni kujitahidi *kila mmoja wetu* kwa uchunguzi na masomo ya Neno la Mungu, kama waumini wa Berea ambao ni "wazuri" na waliosifiwa sana waliochunguza Maandiko kuona maneno ya Paulo-

***"Wakawa wanayachunguza Maandiko*** *kila siku**, ili kuona kama yale waliyosema Paulo na Sila yalikuwa kweli." ( Matendo ya Mitume 17:11)***

Katika nyakati za sasa Biblia haiweki tofauti kati ya makuhani na watu wa kawaida. Hayo yalimalizika wakati Sheria ilipomalizika. Wajibu wakuyachunguza maandiko ni wa mtu binafsi. Njia bora -na ya pekee- ya kufikia uamuzi thabiti ya ukweli wa Biblia ni kujifunza Biblia kwa unyenyekevu, kwa sala na kwa uaminifu. Tunamkaribia Mungu na Kristo kwa kufanya shughuli hii; tunaposoma tunatambua kuwa akili asili ya mwanadamu pasi na mwelekeo huu wa Mungu haina sheria wala haiwezi kudhibitiwa.

Tunapojifunza Biblia, tunapaswa kuutafuta usaidizi wa Mungu kwa sala. Ni muhimu kuelewa kuwa ni Mungu Anayetupa hekima kwa mambo haya na Anaweza kufungua akili zetu ili tuuone uzuri wa Neno Lake, tukimtafuta kwa unyenyekevu. Tutatambua kuwa kusudi ya mambo yote ni kuujaza ulimwengu na utukufu wa Mungu, na kuwa sisi tumependelewa kama njia Anayoitumia kufikia Lengo hilo, tukifanya kazi pamoja Naye, na tukimtii kikamilifu.

***"Bwana asipoijenga nyumba Waijengao wafanya kazi bure" (Zaburi 127:1)***

Lakini Paulo anatuhakikishia ya kwamba:

***"Kazi mnayofanya katika utumishi wa Bwana haitapotea bure." (1 Wakorintho 15:58)***

Tunapojifunza Biblia, tunapaswa kuisoma kwa makini, na kuweka mawazo yetu juu ya kila neno na kujitahidi kuelewa uhusiano wa mstari mmoja hadi mwingine. Tunapojifunza Neno la Mungu, ni sharti tutake kujua na KUTII ukweli. Kwa upande wetu lazima tuwe na hamu kubwa ya kupeleleza kurasa zake ili tuwe na ujuzi kuhusu ujumbe wake wa upendo kuhusiana na Njia ya Uzima.

Kwanza, lazima tuikubali Biblia kama Ujumbe wa Mungu ulioongozwa na Mungu, Ujumbe wa Mungu kwa mwanadamu ulio sahihi bila hitilafu. Lazima tuamini hakika kwamba –

*"Mungu yuko, na kwamba huwatuza wale wanaomtafuta." (Waebrania 11:6)*

Ushahidi zaidi utaimarisha imani yetu ya ukweli wa mapendekezo haya, tunapoendela kujifunza Biblia tunaona ushahidi wa ndani wa ukweli wake na uungu, na uhakika wa maneno yake ya unabii. Kutokana na yale Mungu amefanya, tutaamini kwamba yale ambayo Hajayafanikisha bado ulimwenguni ndio njia ya pekee ya wokovu wa mwanadamu mwenyewe na mwisho wake halisi.

Kwa uchunguzu wetu wa jambo hili, tutajifunza kwamba kitabu hiki, Biblia, hakizungumzi kama vitabu vingine, lakini kinaongea kwa mamlaka kamili, kwa maneno kama vile: *" Bwana Mwenyezi Mungu asema"* na *"Itatokea …"*

Biblia ni mkusanyiko wa vitabu kadhaa, iliyoandikwa na watu wengi tofauti kwa muda mrefu: karibu miaka 1500. Nyakati na mazingira ya kuandikwa kwake – vipindi vya ustawi, na uhamisho, na utumwa- zinaungana, chini ya mwelekeo wa Mungu kuleta ujumbe mmoja kutoka kitabu kimoja hadi kingine: inayoonyesha mpango thabiti wa wokovu, na kuonyesha haja ya mwanadamu ya huruma ya Mungu na wokovu, hauwezi kupatikana kwa juhudi zao. Mungu ndiye mwandishi peke wa kazi hii inayoitwa Biblia.

## MWANZO HADI KUMBUKUKU LA TORATI

Vitabu vya kwanza vitano (Mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati) viliandikwa na Musa, mtoa sheria mkuu wa Israeli. Ni vya umuhimu wa kwanza kwa sababu vinaunda msingi wa yote yanayofuata. Hapa tunajifunza uumbaji wa dunia, na kuuenea kwa wanyama na wanadamu duniani.

Tunajifunza kuhusu kuuanguka kwa kusikitisha kwa mwanadamu, adhabu yake, na mpango wa upendo wa Mungu kwa ukombozi wake; na tena kuhusu kushindwa kwa mwanadamu wakati wa Nuhu. Tunaona mwanzo wa kabila la Wayahudi, na Ibrahimu, na kuteuliwa kwao kama "watu wa kipekee" kwa huduma na utumishi wa Mungu.

*"Kwa maana ninyi ni watu watakatifu kwa Yehova Mungu wenu, naye Yehova amewachagua ninyi* ***muwe watu wake****, mali ya pekee, kutoka kati ya vikundi vyote vya watu vilivyo kwenye uso wa nchi."(Kumb 14:2)*

Tunapata katika vitabu hivi vya Musa sheria ambayo Mungu aliwapa Waisraeli kudhibiti kuwepo kwao kama taifa, hata hivyo inafundisha masomo ya juu kuhusu ujio wa Mwokozi wa wanadamu wote na ambayo inaweka wazi kabisa dhambi mbaya zaidi ya dhambi machoni pa Mungu. Ulimwengu wa sasa, kwa "hekima"wanayojidai nayo, kwa ujumla linatilia shaka maneno ya Musa. Lakini tutajifunza kuwa *hatuwezi kuwa na Kristo bila Musa-*

*"Lakini akamwambia, 'Ikiwa hawamsikilizi Musa na Manabii, wala hawatasadikishwa ikiwa mtu fulani atafufuliwa kutoka kwa wafu."(Luka 16:31)*

*"Naye akaanzia Musa na Manabii wote, akawafasiria mambo yanayomhusu yeye mwenyewe katika Maandiko yote."(Luka 24:27)*

*"Kwa kweli, ikiwa mngalimwamini Musa mngaliniamini mimi, kwa maana huyo aliandika juu yangu. Lakini ikiwa hamyaamini maandishi yake huyo, mtawezaje kuyaamini maneno yangu?"(Yohana 5:46-47)*

Kama Musa sio wa kweli, basi Kristo sio wa kweli vile vile. Maana wao husimama au kuanguka pamoja.

## JOSHUA HADI ESTA

Vitabu 12 vinavyofuata (Joshua hadi Esta) vinaonyesha historia ya Israeli kwa miaka 1000. Ila ni zaidi ya historia tu. Vinafunua mtazamo wa Mungu, mapenzi na kanuni zake katika kushughulika na watu na mataifa. Tunajifunza kumpenda Mungu na kumheshimu Yeye na yote Aliyoyafanya na Anayoyafanya.

## AYUBU

Kitabu cha Ayubu kinaonyesha jinsi Mungu anawaadhibu wana wake wa kweli; Hawaachi bali anawatakasa na kuwasafisha kama dhahabu.

## ZABURI HADI WIMBO ULIO BORA

Zaburi, Mithali, Mhubiri na Wimbo ulio Bora ni ujumbe wa hekima ulioongozwa na Mungu, kuonyesha tabia inayokubalika.

**ISAYA HADI MALAKI**

Vitabu vya unabi,17 kwa idadi (Isaya hadi Malaki), ujumbe wa Mungu kwa Israeli kama taifa, kama maonyo ya hukumu ijayo kwa sababu ya kutomtii Mungu; lakini pia ujumbe wa furaha itakayofunuliwa siku ambayo Israeli na ulimwengu mzima utafurahia baraka na amani. Utekelezaji wa unabii juu ya Israeli katika *kueneza* kwao duniani kote kunatuhakikishia matumaini ya ujumbe huo, siku ambayo Yesu atarudi kubariki mataifa yote,*ulimwenguni*, inakaribia.

**MATHAYO HADI YOHANA**

Tukiangalia ukurasa mwingine katika Agano Jipya, tunapata vitabu 4 vya kwanza ambavyo ni Rekodi za Injili za maisha ya Kristo (Mathayo hadi Yohana), vinafunua udhihirisho wa Mungu katika Mwanawe, kutuonyesha njia, au namna ya maisha na kuendeleza tabia ya Mungu.

“KWA HIYO INAWAPASA NINYI MUWE WAKAMILIFU KAMA BABA YENU WA MBINGUNI ALIVYO MKAMILIFU.” (MATAYO 5:48)

**MATENDO YA MITUME**

Kitabu cha Matendo kinaonyesho matumizi asili ya amri za Yesu-

*“Nendeni ulimwenguni kote, mkawahubirie watu wote Habari Njema. Ye yote atakayeamini na kubatizwa ataokolewa. Lakini ye yote ambaye atakataa kuamini, atahukumiwa”(Marko 16:15-16)*

Tunajifunza kutoka kwa kitabu hiki maana hasa ya kujitolea maisha yetu katika yote tunayofanya ili kumtumikia Mungu na Ukweli wake bali siyo sisi wenyewe au radhi zetu.

**WARUMI HADI YUDA**

Nyaraka 21 (Warumi hadi Yuda) ambazo zinajumuisha nyaraka kwa eklezia mbali mbali na watu binafsi na mitume wa Yesu, kuelezea ukweli wa msingi wa Injili, madhumuni ya kimungu na wanadamu; na kutuonyesha njia ya maisha ya kimungu, kutufundisha na kutuongoza kwa shughuli za kila siku kwa kutangamana kwetu sisi kwa sisi na Mungu pia.

**UFUNUO**

Kitabu cha mwisho, Ufunuo wa Yesu Kristo kinatoa mtazamo wa karibu miaka 2000 ya historia ya dunia, tangu siku za Mitume hadi kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu duniani. Inaonyeshwa kwa ishara na alama ambazo maana na matumizi yake tunajifunza kutoka sehemu nyingine za

Biblia, na imeundwa kufundisha Watumishi wa Mungu kuhusu matukio ya ulimwengu, ili waweze kutambua ishara za nyakati.

**UJUMBE THABITI**

Biblia sio chochote chini ya muujiza wa Fasihi! Ingawa inajumuisha vitabu 66, vilivyo andikwa kwa kipindi cha karne nyingi, na waandishi mbali mbali kutoka kwa wafalme hadi wachungaji, inazungumzia mandhari moja kote, inayofanyika kwa kipindi kirefu kuhusu nia ya milele ya Mungu. Tabia yake na umoja wake unadhihirisha kuwa chanzo chake sio cha uwezekano wa binadamu, na unathibitisha ukweli kwamba –

*"Andiko lote limeongozwa na roho ya Mungu" (2 Timotheo 3:16)*

Wengi wa waandishi walifunga ushahidi wao na Mungu kwa damu yao kumwagwa na adui zao. Njia pekee ya kuzingatia Biblia ni kuona- katika muundo wake, na uhifadhi wake tangu karne zile hadi wakati wetu,- mkono mkuu wa kuongoza unaohamasisha na kudhibiti maandishi ya waandishi wake, na kusababisha muelewano kamili katika rekodi zao zote. Haiwezekani kuitazama Biblia kwa njia nyingine yeyote.

Biblia inaweza kueleweka na mtu anayemtafuta Mungu kwa imani nyenyekevu bila kuhitaji mafunzo ya kitheolojia au ya kanisa katika vyuo vikuu au semina. Taasisi hizo zinazalisha makuhani au makasisi walioelimishwa au waliofundishwa kuhubiri mafundisho fulani ya madhehebu yao; ambao vitabu vyao ni mazao ya vizazi vya mila, badala ya ujumbe wa Biblia.

Hatupaswi kuwacha – *tusidhubutu kuwacha* – ufahamu wetu wa kanuni za Biblia kwa viongozi wa dini. Lazima *tujizamishe* kwenye kurasa zake kwa sala, maombi ya unyenyekevu kwa Mungu ili afungue kuelewa kwetu. Uchunguzi wa kibinafsi kwa namna hii itapanua mawazo yetu kwa uzuri na kusudi la Neno la Mungu.

Soma Biblia kila siku na kwa makini. Tumia mafunzo ya Biblia ya kila siku yaliyopendekezwa katika kijitabu hiki, *The Bible Companion*. Isome kwa uaminifu, na utasoma Agano la Kale mara moja kwa mwaka, na Agano Jipya mara mbili kila mwaka.

Ikiwa kuna kitabu chenye mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa na mpango wa Baraka za milele kwa mtu, **NI BIBLIA**. Haina ushindani. Kama haitangazi njia ya uzima, hakuna kinachofanya hivyo. Biblia inawapa wote wanaoisoma kwa uaminifu furaha na hekima.Mungu anawaita watu waache dunia ili wawe sehemu ya jamii Yake. kwa kila ujuzi unaopata kutoka katika Biblia, unazidi kupata kuajibika kwa Mwenyezi Mungu. pendekezo letu kwa watu ni kuu. Inahitaji mtu anayejifunza kupokea huu mwito kutoka kwa Mola.

*Somo lifuatalo- Biblia: Jinsi Ilivyotujia.*

Jina Bw/Bi ………………………………………………………………………………
Anwani ……………………………………………….. Msimbo wa posta ……………….

*Unaweza kuhitaji karatasi ya ziada kwa majibu yako iwapo hakuna nafasi ya kutosha hapo chini. Hii itakusaidia wewe – na sisi – kujua kiasi gani ulichogundua kuhusu Biblia yako. Tafadhali rejesha fomu hii kwenye bahasha zilizotolewa hata kama huwezi kujibu maswali yote. Tunapopokea tutaendelea kujifunza zaidi.

**MASWALI KUHUSU SOMO HILI**

1. Ni nini kusudi la mwisho na muhimu zaidi katika Uumbaji, na katika ufunuo wa Mungu katika Biblia?
2. Je ni hali gani ya akili tunapaswa kuwa nayo tunapojifunza Biblia?
3. Je, jukumu letu ni nini mara tu tunapopata ujuzi wa kusudi la Mungu?
4. Biblia ni tofauti na vitabu vya duniani kwa njia gani?
5. (a) Vitabu vya kwanza 5 viliandikwa na nani?
   (b) Eleza mambo 3 tunayojifunza kutoka kwa vitabu hivi.
6. Tuna ushahidi gani katika Agano Jipya kutuhimiza kuamini maneno ya Musa?
7. Vitabu vya Yoshua hadi Esta vinaonyesha nini?
8. Nini kichwa cha vitabu vya Unabii?
9. Kumbukumbu za Injili zinasema nini?
10. Ni nini kinachoonyeshwa katika kitabu cha Ufunuo?
11. Tunajifunza nini kuhusu Biblia na ukweli kwamba *iliandikwa* miaka mingi na waandishi tofauti, bado wanaelezea kusudi thabiti na isiyobadilika?
12. Kwa nini hatuwezi kuwacha mafundisho yetu ya kidini kwa makasisi wa makanisa au makuhani?